# HABARI na MATUKIO

Toleo Na. 3 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Mei 2022

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA

# TFRA yaainisha mikakati kuhakikisha wakulima wanapata mbolea



Wajumbe wa bodi ya wakurugenzi inayosimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) wakiongozwa na mwenyekiti wake Prof. Prof. Anthony Mshandete (wanne kutoka kulia) na menejimenti ya (TFRA) wakipewa maelezo na Mkurugenzi wa masuala ya kiufundi katika kiwanda cha mbolea Intracom Jijini Dodoma Victor Ngendanzi walipofanya ziara kiwandani hapo jana tarehe 29 Aprili, 2022.

## NDANI>>

**Elimu ya matumizi ya mbolea kupunguza kilimo cha kuhamahama Lindi** 6

**YALIYOZUNGUMZWA NA VIONGOZI WA KITAIFA UZINDUZI WA UGAWAJI VITENDEA KAZI ...** 12

**TFRA kanda ya kaskazini yaendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wasimamizi...** 19

# Mashamba darasa yafungua milango ya biashara na matumzi sahihi ya mbolea Lindi, Mtwara

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa mujibu wa Sheria ya mbolea ya mwaka 2009 pamoja na kanuni zake za mwaka 2011 na marekebisho yake ya mwaka 2017 imepewa jukumu la kutoa elimu kwa kushirikiana na Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu matumizi sahihi ya mbolea.

Shughuli ya uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea katika Mkoa wa Lindi na Mtwara ilianza mwezi Mei, 2021 na ilifanyika kwa kutumia mbinu ya mashamba darasa kwa ushirikiano wa Sekretarieti hizo, Halmashauri za Wilaya ya Ruangwa, Mtama, Mtwara na Masasi ambapo jumla ya wakulima 75 walishiriki katika kuandaa, kuyatunza na kuyaendesha mashamba darasa kwa mazao ya Mpunga na mahindi. Uhamasishaji huo uliotumia mfumo wa mashamba darasa umehitimishwa kwa kuwa na kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mkulima ambapo wakulima kutoka maeneo mbalimbali wanaalikwa kujifunza kwa kuona namna matumizi sahihi ya mbolea yameweza kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Uzinduzi wa kampeni ya uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea ulifanyika tarehe 11, Januari 2021 katika kijiji cha Mnolela Halmashauri ya Mtama mkoani Lindi kwa lengo la kuwahamasisha wakulima wa Lindi na Mtwara kuzingatia kilimo cha kisasa cha matumizi sahihi ya mbolea.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, alikuwa ni shuhuda wa kwanza wa uzinduzi wa kampeni hiyo na kukiri wazi kwamba matumizi ya mbolea katika mikoa ya Lindi na Mtwara yapo chini na kwamba kunahitajika jitihada za makusudi kuwahamsisha wananchi kuboresha kilimo chao.

Wazo la kuweka msukumo wa matumizi wa mbolea katika mikoa ya Lindi na Mtwara lilibuniwa na TFRA baada ya tathmini iliyofanywa kuonyesha kuwa matumizi ya bidhaa hiyo muhimu kwa kilimo yako chini sana ikilinganishwa na mikoa mingine ya Tanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dkt Stephan Ngailo anasema uhamasishaji wa matumzi ya mbolea katika mikoa hiyo utakuwa ni suala endelevu kwa kuhakikisha kwamba wakulima wana uelewa mpana wa kujifunza kwa vitendo faida na hasara za kutumia au kutokutumia mbolea katika shughuli za kilimo.

Zaidi ya wakulima 60 waligawiwa mbegu na mbolea kwa ajili ya kutumia kwenye mashamba yao binafsi ikiwa ni jitihda za serikali kuendeleza uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

Dhima ya uhamasishaji wa matumizi ya mbolea katika mikoa ya kusini inatokana na upanuzi na maboresho yaliyofanyika katika bandari ya Mtwara ambayo yanatoa fursa mbalimbali kwa mikoa ya Lindi na Mtwara kutumia bandari hiyo kuingiza mbolea kwa wingi ili iwafikie wakulima kwa bei nafuu. Kampeni ya uhamasishaji matumizi ya mbolea kupitia mashamba darasa inaaminika itaongeza mahitaji ya bidhaa hiyo kwa mikoa jirani ya Ruvuma na Njombe.

Kwa ujumla mikoa ya Lindi na Mtwara ina matumizi madogo ya mbolea nchini. Moja ya sababu kubwa ni uelewa mdogo wa wakulima kuhusu matumizi ya bidhaa hiyo, kwa mujibu wa wataalam wa kilimo.

Baada ya kukamilisha mafunzo kupitia mashamba darasa, Mamlaka kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa ya Lindi na Mtwara, Halmashauri husika na wakulima ilianda kilele cha siku ya mkulima katika halmashauri ya Ruangwa na Mtwara DC kwa lengo la kuhitimisha shughuli hiyo. Kauli mbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa "TUMIA MBOLEA KUONGEZA KIPATO NA TIJA" ambapo katika mkoa wa Lindi ilifanyika tarehe 11.04.2022 na Mgeni Rasmi alikuwa Mkuu wa Mkoa Mhe. Zainab Taleck wakati Mkoa wa Mtwara maadhimisho hayo yalifanyika tarehe 13.04.2022 na mgeni rasmi akiwa Mhe. Kyoba Mkuu wa Wilaya ya Mtwara aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Brigedia Jenerali Marco Gaguti.

Kampeni ya uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea ya Katika mikoa ya lindi na mtwara imepokelewa vema na wakulima pamoja na viongozi wa ngazi zote katika mikoa yote miwili ya Lindi na Mtwara. Hivyo inatarajiwa kuwa mwitikio uliooneshwa na wakulima utasaidia kuongeza matumizi ya mbolea katika mikoa hivyo na hatimaye kuongea tija na uzalishaji wa mazao ya chakula.

***Anuani***
***Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA)***
***Mtaa wa Kilimo, Jengo la Kilimo,***
***S.L.P 46238 DAR ES SALAAM***
***+255 22 2861939***

Tanzania Fertilizer Regulatory Authority tfra_official tfra_official

# TFRA yaainisha mikakati kuhakikisha wakulima wanapata mbolea

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi inayosimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Prof. Anthony Mshandete ameweka wazi mikakati mahususi ya kuhakikisha wakulima nchini wanapata mbolea bora kwa ajili ya matumizi ya kilimo.



Wajumbe wa bodi ya wakurugenzi inayosimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) wakiongozwa na mwenyekiti wake Prof. Prof. Anthony Mshandete (wanne kutoka kulia) na menejimenti ya (TFRA) wakipewa maelezo na Mkurugenzi wa masuala ya kiufundi katika kiwanda cha mbolea Intracom Jijini Dodoma Victor Ngendanzi walipofanya ziara kiwandani hapo jana tarehe 29 Aprili, 2022.

Ameeleza mikakati hiyo jana tarehe 29 Aprili, 2022 ambapo wajumbe wa Bodi ya TFRA pamoja na watendaji wa mamlaka hiyo walitembelea eneo kinapojengwa kiwanda hicho kwa lengo la kujionea hatua na maendeleo ya ujenzi wa kiwanda kinachotarajia kuanza uzalishaji wa tani 6000 za mbolea mwezi Julai 2022.

Akieleza mikakati hiyo, Prof. Mshandete alisema mkakati wa kwanza ni kuhakisha mbolea inayozalishwa inakuwa na ubora na viwango vinavyokubalika nchini. Alisema wananchi wakiona ubora wa mbolea inayozalishwa na kiwanda hicho itakuwa rahisi kwa kiwanda kujitangaza na mbolea itauzika kiurahisi.

Akielezea mkakati wa pili Prof. Mshandete alisema ni uongozi wa kiwanda kuwa na mkakati wa mawasiliano kwa ajili ya kutangaza aina ya mbolea itakayokuwa ikizalishwa na kiwanda hicho yenye mchanganyiko wa samadi na madini mengine kama phosphate na chokaa tofauti na aina zilizozoeleka kwa wakulima nchini.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi inayosimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Prof. Anthony Mshandete (wa pili kulia) akihoji jambo kwa Mkurugenzi wa masuala ya kiufundi katika kiwanda cha mbolea Intracom Jijini Dodoma Victor Ngendanzi walipofanya ziara kiwandani hapo kukagua maendeleo ya ujenzi wa kiwanda hicho.

Prof. Mshandete alisema kutokana na ukweli kwamba mbolea inayozalishwa kiwandani hapo kuwa mpya kwenye soko la ndani elimu kuhusu ubora wa mbolea hiyo unapaswa kutolewa ili wananchi waweze kuifahamu na kuwa na utayari wa kuitumia na hivyo kupunguza changamoto ya upatikanaji wa mbolea nchini.

Aidha, Prof. Mshandete amewataka wasimamizi wa kiwanda cha Itracom Fertilizer LTD kuwa na hari (aggressiveness) katika kutangaza bidhaa na kuwashauri kushiriki katika maadhimisho ya siku ya mbolea yanayotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu ili kuwapa fursa ya kuitangaza bidhaa hiyo.

# TFRA yaainisha mikakati kuhakikisha wakulima wanapata mbolea

Akizungumzia suala la upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea kiwandani hapo Prof. Mshandete alisema kutatokana na namna nzuri ya kutangaza uwepo wa kiwanda hicho pamoja na kutangaza malighafi zinazotumika katika uzalishaji kutakakofanywa na mwekezaji huyo.

Pamoja na hayo Prof. Mshandete ametoa wito kwa mwekezaji Itracom Fertilizer LTD kutosita kuishirikisha TFRA na mamlaka nyingine za serikali pindi wanapokutana na changamoto wakati wa utekelezaji wa mradi huo.

Akizungumza kwa upande wa mwekezaji, Dr. Ntukamazina Nepomuscene Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu wa Itracom Fertilizer LTD alisema ujenzi wa kiwanda upo katika hatua nzuri ambapo mitambo imeshaanza kufungwa tayari kuanza uzalishaji ifikapo Julai 2022.



Baadhi ya mitambo iliyopo kwenye kiwanda cha mbolea cha Intracom Fertilizer Limited Kinachojengwa jijini Dodoma

Aliongeza kuwa, tayari kiasi kikubwa cha samadi kimepatikana na kimefikishwa kiwandani hapo kwa ajili ya kuanza uzalishaji wa mbolea hiyo.

Uwekezaji huo utakaogharimu kiasi cha dola za kimarekani Milioni 180 ni matokeo ya ziara ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan nchini Burundi na kueleza fursa za uwekezaji zilizopo nchini na kumpata mwekezaji wa kiwanda cha Intracom Fertilizers Limited.



wenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi inayosimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Prof. Anthony Mshandete (wa pili kulia) akiangalia na kufuatilia maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa masuala ya kiufundi katika kiwanda cha mbolea Intracom Jijini Dodoma Victor Ngendanzi katika moja ya eneo zilipo mashine walipofanya ziara kiwandani hapo tarehe 29 Aprili, 2022



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi inayosimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Prof. Anthony Mshandete, wajumbe wa bodi na Menejimenti ya TFRA wakifuatilia maelezo ya Mkurugenzi wa masuala ya kiufundi katika kiwanda cha mbolea Intracom Jijini Dodoma Victor Ngendanzi.

# TFRA yaainisha mikakati kuhakikisha wakulima wanapata mbolea











# Elimu ya matumizi ya mbolea kupunguza kilimo cha kuhamahama Lindi

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack amesema uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima wa mkoa wa Lindi kutapunguza utamaduni wa kilimo cha kuhamahama kwa wananchi wa Mkoa huo.

Amesema, wananchi wake wamekuwa wakihamahama kutokana na kuamini kwamba shamba likilimwa linapoteza rutuba na kupelekea wananchi hao kulima mara moja na kuhamia eneo lingine wakiamini kuwa eneo ambalo halikulimwa linakuwa na rutuba ya kutosha kustawisha mazao.

Kauli hiyo aliitoa tarehe 11 Aprili, 2022 alipokuwa akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mkulima yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA).

“Kwa hili la uhamasishaji wa matumizi ya mbolea mlilolileta naaamini kuwa sasa wananchi wetu watakuwa na makazi ya kudumu. Sasa tuwape uhakika kwamba kwenye ardhi hiyohiyo wakilima kwa kutumia mbolea watavuna mazao ya kutosha”. Telack aliongeza.



Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Bi. Zainab Telack akivuna muhindi katika moja ya shamba lililopandwa kwa mbolea ili kudhibitisha tija iliyotokana na kupanda kwa kutumia mbolea katika eneo la Chimbila B Wilaya ya Luangwa mkoani Lindi leo tarehe 11 Aprili, 2022

Maadhimisho hayo ni kilele cha uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima wa mkoa wa Lindi yaliyoanza mwezi Mei, 2021 kufuatia mkoa huo kuwa na matumizi hafifu ya mbolea ukilinganisha na maeneo mengine ya nchi kama vile Iringa, Mbeya, Mwanza na maeneo mengine.

Akizungumzia sababu zinazopelekea uwepo wa matumizi hafifu ya mbolea kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi, Telack alisema ni kutokuwepo kwa wauzaji wa mbolea katika mikoa ya kusini na kuyataka makampuni yanayojihusisha na biashara ya mbolea kufungua matawi ili kuwawezesha wakulima wa maeneo hayo kupata huduma hiyo.

“Tunahitaji elimu, tunahitaji kusaidiwa na ili mtusaidie kwa uharaka leteni tawi karibu, tuwasaidie wakulima naomba tuwasaidie wakulima” Telack alisisitiza.

Kwa upande wa huduma ya upimaji wa afya ya udongo inayoweza kuwasaidia wakulima kujua aina ya udongo na mazao yanayoweza kustawi Telack aliitaka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) kufungua tawi katika mkoa huo ili kuwezesha wananchi kupata huduma hiyo.

Aidha, Mkuu wa Mkoa Telack aliwaelekeza wakurugenzi wa halmashauri kuwekeza kwa wakulima na kuhakikisha mazao wanayolima yanawekwa mbolea na wanaongeze tija.

# Elimu ya matumizi ya mbolea kupunguza kilimo cha kuhamahama Lindi

Akinukuu kauli ya Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) alisema, Wewe ulisema kuona ni kuamini na mimi nasema kuona ni kujifunza na sisi tumejifunza na kuwataka wakulima waliopata elimu hiyo kufikisha utaalamu huo kwa wakulima wengine ili na wao wapate elimu hiyo.



Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Bi. Zainab Telack akifuatilia maelezo ya aina za mbolea kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo.

Akihitimisha hotuba yake, Bi. Telack alisema, kwa sababu Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan amewekeza na sisi tuwekeze, naomba sasa tuwekeze kwa wakulima ili mhe. Rais aone tija inayotokana na uwekezaji alioufanya kwenye Sekta ya Kilimo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TFRA, Dkt. Ngailo alisema mamlaka iliamua kufanya uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea katika mikoa ya Lindi na Mtwara kutokana na maeneo hayo kutojihusisha na matumizi ya mbolea kwenye shughuli zao za kilimo.

Alisema, hiyo ni hatua ya awali katika uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea itakayopelekea wadau na wafanyabiashara wa mbolea kufungua biashara ya mbolea katika mikoa ya Kusini yaani Lindi na Mtwara.



Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Bi. Zainab Telack (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wanakikundi cha Jitegemee wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya mkulima tarehe 11 Aprili, 2022 wilayani Ruangwa mkoani Lindi.

Dkt. Ngailo aliongeza kuwa, kufuatia uwepo wa bandari ya Mtwara itarahisisha usafirishaji wa mbolea kutoka nje ya nchi na kushushwa moja kwa moja kwenye bandari hiyo hivyo kuwapunguzia wakulima adha ya upatikanaji wa mbolea.

“Tumeona kuanzishwa mashamba darasa ni njia sahihi ya kuwahamasisha wakulima kutumia mbolea katika kilimo kwani vikundi vya wakulima vilishiriki mwanzo mpaka mwisho katika kuhudumia mashamba darasa hayo” Dkt. Ngailo alisisitiza

Kwa upande wa vikundi vya wakulima kupitia risala yao walieleza manufaa waliyoyapata kufuatia elimu ya matumizi sahihi ya mbolea na namna walivyohusika katika maandalizi mpaka mavuno ya mazao hayo.



Mkuu wa Mkoa wa Lindi, ZainabTelack (wa Tatu kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na wawakilishi wa makampuni ya mbolea yaliyoshiriki katika kilele cha Siku ya Mkulima wilayani Ruangwa mkoani Lindi



Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Bi. Zainab Telack (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) walioshiriki katika shughuli ya uhamasishaji wa matumizi ya mbolea kwa wakulima wa mkoa wa Lindi.





Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo (wa nne kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi walioshiriki katika shughuli ya uhamasishaji wa matumizi ya mbolea kwa wakulima wa Mkoa wa Lindi.



Mkuu wa mkoa wa Lindi, Bi. Zainab Telack akimsikiliza mwanakikundi wa Jitegemee Bi. Samia Ngajua akitoa shuhuda wa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea waliyoipata kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) walipokuwa wakitoa elimu hiyo kupitia mashamba darasa yaliyoanzishwa kwa madhumuni hayo.



Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Bi. Zainab Telack (kushoto) akifuatilia maelezo kutoka kwa Kaimu Meneja wa Ukaguzi kutoka TFRA, Dkt. Asheri Kalala alipokuwa akikagua mashamba darasa yaliyolimwa kwa kutumia mbolea na yale ambayo hayajatumia mbolea leo tarehe 11 Aprili, 2022.

# Matumizi ya mbolea yako chini mkoani Mtwara, hutumia tani 997 pekee kwa mwaka

## TFRA yapongezwa kwa uhamasishaji matumizi sahihi ya mbolea

Imeelezwa kwamba Mkoa wa Mtwara umekuwa ukitumia wastani wa tani 997 za mbolea ambacho ni kiasi kidogo ukilinganisha na mahitaji ya lengo la mkoa la kutumia kiasi cha tani 2000 kwa mwaka.

Hivyo uwepo wa mashamba darasa ya kuhamasisha matumizi ya mbolea yanayosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) yamekuja wakati muafaka kwani mkoa upo katika utekelezaji wa mkakati wake wa kuongeza uzalishaji na tija.



Mgeni rasmi, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Dunstan Kyobya akihutubia umati kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Brigedia Jenerali Marco Gaguti wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mkulima yaliyofanyika tarehe 13 Aprili, 2022 katika Kijiji cha Lolido Kata ya Kitere Mkoani Mtwara.




Mgeni rasmi Dunstan Kyobya akitoa maelekezo kwa wajumbe alioambatana nao (hawapo pichani) wakati akiwa katika scheme ya Mpunga ya Kitere lilipo shamba darasa la mtumizi sahihi ya mbolea wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mkulima yaliyofanyika tarehe 13 Aprili, 2022 katika Kijiji cha Lolido Kata ya Kitere Mkoani Mtwara.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Dunstan Kyoba kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti alipokuwa akitoa hotuba wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mkulima yaliyofanyika katika Kijiji cha Lolido Kata ya Kitere Mkoani Mtwara tarehe 13 Aprili, 2022.

Kyoba alisema, baada ya kujionea utofauti wa shamba la Mpunga uliopandwa kwa kutumia mbolea na ule usiotumia mbolea katika mashamba darasa yaliyopo kwenye scheme ya Kitere amewataka wakulima kufanya kwa vitendo kwenye mashamba yao yale waliyojifunza kupitia

# Matumizi ya mbolea yako chini mkoani Mtwara, hutumia tani 997 pekee kwa mwaka

mashamba darasa hayo ili kuongeza tija, uzalishaji na kipato

"Na ni kweli, nimetembelea lile shamba kwenye scheme ya Kitere niwapongeze sana TFRA na kikundi cha wakulima 'Tupendane' mmefanya kazi kubwa sana hongereni sana, nimeambiwa kile kipande kimoja cha shamba darasa kilichopandwa kwa mbolea unaweza ukatoa gunia 25 ukienda unaona kabisa lakini lile ambalo halikupandwa kwa mbolea unaona kuwa hakuna kitu kabisa" Kyobya alikazia.

Pamoja na hayo, Kyobya aliwaasa wakulima kuepuka kununua mbolea na pembejeo za kilimo kwenye maduka yasiyo rasmi kwani ikitokea bidhaa iliyonunuliwa ni feki itakuwa ngumu kwa wataalamu kumpata muuzaji na kumchukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

Pia, aliwataka wakulima kuepuka kununua mbolea za kupima kutokana na mbolea hizo kupoteza ubora na hivyo kusababisha hasara na kuwataka wanunue zile zilizofungwa vizuri kama inavyoelekezwa na wataalamu wa kilimo na mwisho wa siku wapate matokeo chanya.

Kufuatia changamoto ya upatikanaji wa maji katika scheme ya Kitere, Kyobya aliielekeza Halmashauri ya Mtwara wakishirikiana na Mamlaka ya maji safi Mtwara kuhakikisha maji yanapatikana muda wote katika scheme hiyo ili kuwaondolea wakulima changamoto ya upatikanaji wa maji kama walivyoomba katika risala yao.



Mgeni rasmi, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Dunstan Kyobya (aliyeweka pamoja mikono) akipongeza juhudi zilizofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania( TFRA) kwa kushirikiana na Afisa Ugani wa Kata, Wilaya na Mkoa katika kuelimisha wananchi wa Kitere juu ya matumizi sahihi ya mbolea ili kuongeza kipato na tija katika shughuli za kilimo.

Akitoa maelekezo kwa TFRA Kyobya aliitaka mamlaka kuhakikisha inawasimamia kikamilifu wafanyabiashara wa mbolea na kuhakikisha mkoa wa




Viongozi wa Wilaya za Mkoa wa Mtwara wakifuatilia kwa makini matukio mbalimbali wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mkulima yaliyofanyika katika Kijiji cha Lolido Kata ya Kitere Mkoani Mtwara tarehe 13 Aprili, 2022. Kutoka kulia ni Claudia Kitta Mkuu wa wilaya ya Masasai, akifuatiwa na Mkuu wa Wilaya ya Newala, Mwangi Rajab Kudya na Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu Mariam Chaurembo.

# Matumizi ya mbolea yako chini mkoani Mtwara, hutumia tani 997 pekee kwa mwaka




Wanakikundi pamoja na wananchi wa Kata ya Kitere wakifuatilia kwa makini matukio yanayoendelea wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mkulima yaliyofanyika tarehe 13 Aprili, 2022 katika Kijiji cha Lolido Kata ya Kitere Mkoani Mtwara.

Mtwara unakuwa na wauzaji na wasambazaji wenye sifa pamoja na kudhibiti bei za mbolea ili kuwawezesha wakulima kumudu bei ya mbolea na kuitumia kama walivyoelimishwa.

Aliwaagiza maafisa ugani kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea na kusimamia usambazaji wake kwa kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo za kilimo kwenye maduka rasmi na wanapewa risiti kuthibitisha manunuzi yao.

“Maafisa ugani mnapaswa kuwa karibu na wakulima ili kuwawezesha kufuata kanuni zote za kilimo ikiwa ni pamoja na kuchagua shamba, kuandaa shamba kwa wakati, kupanda kwa kutumia mbolea sahihi ya kupandia na kwa wakati, kuweka mbolea ya kukuzia na kupalilia kwa wakati.

Alisema shamba likifuata kanuni zote za kilimo huwa na matokeo mazuri na hivyo kuongeza tija na mapato kwa mkulima, halmashauri na taifa kwa ujumla.

Akihitimisha hotuba yake, Kyobya alisema mfumo uliotumiwa na TFRA wa kutumia mashamba darasa ni mzuri kwani unawafikia wadau wengi kwa muda mfupi na kukiri mkoa wa Mtwara umedhamiria kuongeza uzalishaji wa mazao ya mpunga na mahindi hivyo utakuwa karibu na wakulima wakati wote wa kilimo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephani Ngailo aliwatoa hofu wananchi na wakulima nchini kuwa matumizi ya mbolea hayaharibu udongo isipokuwa wazingatie matumizi sahihi ya mbolea kwa kuzingatia afya ya udongo.

Alisema, TFRA itaendelea kushirikiana na sekretarieti za mikoa na halmashauri kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea ili kuongeza tija katika uzalishaji.

Aidha, aliwashukuru wadau wote waliowezesha shughuli ya uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea ikiwa ni pamoja na Mkoa wa mtwara, wakurugenzi wa halmashauri na maafisa kilimo, makampuni ya usambazaji wa mbolea hususan ETG, Premium, OCP pamoja na Yara kwa kutoa mbolea kwa vikundi vya wakulima na kuwezesha kujifunza kwa vitendo.

# YALIYOZUNGUMZWA NA VIONGOZI WA KITAIFA WAKATI WA UZINDUZI WA UGAWAJI VITENDEA KAZI KWA MAAFISA UGANI KILIMO LEO APRILI 4, 2022 JIJINI DODOMA

## Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan

Tutagawa vipima udongo kwenye Halmashauri 143, simu janja pamoja na visanduku vya kutolea huduma 3,300.

Tumefanikisha kufungua masoko mapya ya mazao nje ya nchi hususan zao la parachichi katika nchi za India na Afrika Kusini baada ya kukidhi viwango vya ubora. Pia, tumefanikiwa kupata maghala ya kukodi nje ya nchi kwa ajili ya kuhifadhi nafaka yenye uwezo wa kubeba tani 5,000 nchini Sudan Kusini, tani 2,000 nchini Congo na jitihada hizi zinaendelea ili kufungua maghala mengine China, Vietnam na UAE.

Mimi ni muumini mkubwa kwamba kilimo kinaweza kikaivusha nchi, baadhi ya jitihada tutakazozifanya kuanzia mwaka 2020/21 - 2025/26 kwa ajili ya kutimiza malengo ya kilimo tuliyojiwekea ni kuongeza bajeti ya utafiti kutoka shilingi bilioni 7.35 hadi bilioni 11.

Nawaomba sana vijana wa kitanzania muingie kwenye kilimo na hamtajuta kwani mtatengeneza fedha ya halali mikononi mwenu. Nataka Waziri wa Kilimo, zile 'blocks' mnazozitengeneza mkoani, tengeni pia kwa ajili ya vijana

Serikali iliweka malengo



ya kuweka nguvu kwenye sekta ya kilimo ikiwemo kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta hiyo kwa ujumla wake kutoka 5% hadi 5.7% ambapo Waziri wa Kilimo amesema kuwa kufikia mwaka 2025, sekta hiyo itakua kwa 10%.

Katika hatua nyingine, tumeweza kufanikisha upatikanaji wa Ithibati ya Ubora kwa ajili ya maabara yenye viwango vya ubora vya kimataifa kwa ajili ya Mamlaka ya mimea na viuatilifu, hatua hii itatusaidia kipindi tunachotoa mazao yetu wengine wasitutilie shaka.

Baada ya kujengwa kwa bwawa la umeme Rufiji, kuna eneo linalobakia, nataka likapimwe na ligawiwe ili lianze kuzalisha kulingana na mazao yatakayoweza kuzalishwa katika eneo hilo

Wizara ya Kilimo ihakikishe huduma ya upimaji wa udongo inakua kwa sababu kwa miaka kadhaa tumetumia mbolea mbalimbali ambapo udongo wetu unapungua nguvu hivyo ni vyema kupima udongo kujua uwezo wake na vipi tunaweza kuusaidia kuuongezea nguvu ili uendelee kuzalisha kwa kiasi kikubwa.

Mwaka 2020, tulifanya majaribio ya kutoa ruzuku za pembejeo kwa wakulima ambapo jaribio hilo limetoa matokeo mazuri hivyo nimeelekeza kuwe na Mfuko Maalum wa Pembejeo.

Natoa agizo kwa Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Rais - Utumishi kupitia upya na kufanya mabadiliko ya Muundo wa Tume ya Umwagiliaji maji ili kuhakikisha inakuwa na ofisi katika kila Wilaya, na uwajibikaji wa Maafisa hao uende chini ya ofisi za Wilaya zitakazoanzishwa.

Nawataka Wizara ya Kilimo kuanzisha Mifuko ya mizunguko ambao mmoja utakuwa wa Pembejeo na mwingine utakuwa wa maendeleo ya kilimo.

Tumeelekeza kuanza kujenga maghala maeneo ya vijijiji walipo wakulima ili wanapovuna waweze kuweka mazao yao ndani ya maghala ili kuondoa tatizo la upotevu wa mazao na ili mnunuaji anapokuja

# YALIYOZUNGUMZWA NA VIONGOZI WA KITAIFA WAKATI WA UZINDUZI WA UGAWAJI VITENDEA KAZI KWA MAAFISA UGANI KILIMO LEO APRILI 4, 2022 JIJINI DODOMA

## Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan

ayakute katika hali nzuri.

Aidha, nawataka Wizara ya Kilimo itoe kipaumbele kwa sekta ndogo ya Sukari na kutekeleza mikakati ya kuongeza uzalishaji wa sukari ili tujitosheleze kabisa ifikapo mwaka 2025, nasisitiza uwajibikaji na uwazi kwa viwanda vinavyozalisha sukari.

Mashamba yote ambayo yapo chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo hayazalishi yamekaa tu, yatoke yakazalishe kwani tunapozungumza uanzishwaji wa mashamba makubwa, mashamba haya ni sehemu moja wapo.

Tuangalie hali ya chakula nchini kwani kutokana na mabadiliko ya uchumi nchini, chakula kina mahitaji makubwa sana hivyo tunaweza tukavutika na soko la Dunia tukajisahau kuweka akiba nchini hivyo, naomba tuhakikishe tunajitosheleza kwanza ndipo tupeleke nchi zingine.

Lengo la kuweka maghala haya ni kusukuma mazao yetu yaende sokoni ambapo tayari tumesaini mikataba kadhaa na nchi hizo ili tuweze kupeleka mazao yetu. Tunafanya jitihada zote hizi ili wakulima wetu waweze kupata thamani ya jasho wanalolitoa.

Serikali pia ilipanga kuongeza eneo la umwagiliaji maji kutoka hekta 695,000 hadi milioni 1.2, ila ukiangalia mambo ambayo tayari tumeshayafanya na malengo ambayo wizara iliyojiwekea ya kuongeza au kutumia kilimo cha umwagiliaji maji kutoka 10% hadi 50% tutaweka hekari milioni 18 kwenye umwagiliaji maji.

Malengo mengine ni kuongeza thamani ya mazao tunayoyauza nje kutoka Dola za Marekani bilioni 1.2 hadi Dola za Marekani bilioni 5, kama tukifuata Mpango wa Pili wa Kilimo Tanzania, basi tutavuka lengo hilo tulilojiwekea. Aidha, tulilenga kuongeza idadi ya mashamba makubwa kutoka 110 hadi 1,000.

Sekta ya Kilimo imeendelea kuwa muhimili mkuu na kuhimu wa kukuza uchumi wa Taifa letu na kuleta maendeleo ndani ya nchi yetu ambapo kwa mwaka 2020, sekta hii ilikua kwa 4.9% na kuchangia 26.9% kwenye Pato la Taifa na kutoa ajira kwa Watanzania 61% na kuchangia 65% kwenye malighafi za viwanda.

Pamoja na umuhimu wake mwingine, Sekta ya Kilimo imewezesha kutufanya Tanzania tujitosheleze kwa chakula kwa 100% pia inasaidia kupunguza mfumuko wa bei ndani ya nchi yetu kwani chakula kinapokuwa cha kutosha bei hizo zinashuka.

Serikali inaendelea kuimarisha huduma za Ugani, leo tunagawa pikipiki 6,700 ambapo pikipiki 300 zilishatangulia ambazo zinafanya jumla ya pikipiki kufikia 7,000 kwa Maafisa Ugani wote. Sio uhakika kuwa baada ya miaka miwili pikipiki zitakuwa zenu bali tutawapima kwa kazi mnazozifanya.

Serikali inaendelea kuimarisha huduma za Ugani, leo tunagawa pikipiki 6,700 ambapo pikipiki 300 zilishatangulia ambazo zinafanya jumla ya pikipiki kufikia 7,000 kwa Maafisa Ugani wote. Sio uhakika kuwa baada ya miaka miwili pikipiki zitakuwa zenu bali tutawapima kwa kazi mnazozifanya ndipo Afisa anaweza kupewa ikawa mali yake.

Jitihada zingine ni kuongeza bajeti ya huduma za Ugani kutoka shilingi bilioni 17.7 hadi shilingi bilioni 51.45, kuongeza fedha za uzalishaji wa mbegu kutoka shilingi bilioni 5.42 hadi shilingi bilioni 10.58, sambamba na kuongeza bajeti hiyo, tumewezesha NFRA na Bodi ya Mazao Mchanganyiko kwa jumla ya shilingi bilioni 129 ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

# YALIYOZUNGUMZWA NA VIONGOZI WA KITAIFA WAKATI WA UZINDUZI WA UGAWAJI VITENDEA KAZI KWA MAAFISA UGANI KILIMO LEO APRILI 4, 2022 JIJINI DODOMA

## Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa



Mafanikio yaliyotajwa na Waziri wa Kilimo ni sehemu ya maelekezo ya Rais wetu, Mhe. Samia Suluhu Hassan, lakini pia nakuhakikishia Mhe. Rais

kazi inayofanywa na Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe ni nzuri na inaleta matumaini.

## Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - TAMISEMI, Mhe. Innocent Bashungwa



Kupitia tukio hili kubwa la kihistoria na uongozi wako tunaenda kuleta mageuzi makubwa kwa wakulima wetu.

Sisi Ofisi ya Rais TAMISEMI tayari tumefanya vikao na wataalam wetu na tutatekeleza maagizo yote uliyotupatia, sasa hakuna visingizio baada ya vitendea kazi hivi kupatikana.

## Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe



Taifa letu limeajiri watanzania 61% ambao wapo mashambani wanashughilika na uzalishaji na 15% hadi 20% wanashughulika na mnyororo wa thamani wa Sekta ya Kilimo. Sekta ya Kilimo inachangia wastani wa 25% hadi 27% wa Pato la Taifa.

Tanzania ina eneo linalofaa kwa kilimo Hekta milioni 44 na linalofaa kwa umwagiliaji Hekta milioni 29, sisi kama nchi tunajitosheleza kwa chakula. Hadi kufika mwaka 2050, dunia itakua na watu zaidi ya bilioni 9, Africa bilioni 2 na Tanzania milioni 100. Biashara ya kilimo katika soko la Afrika inatarajiwa kuwa na Dola Trilioni 1 hadi kufika mwaka 2030 na sisi kama nchi tuna uwezo wakuilisha Afrika na kuchangamkia fursa katika eneo hili la biashara ya kilimo.

Tija katika Sekta ya Kilimo inatokana na utafiti, Mhe. Rais umetuongezea bajeti ya Utafiti kwa mwaka huu wa fedha kutoka shilingi bilioni 7 hadi bilioni 11.

Tumeanza utaratibu wa kuwapa elimu Maafisa Ugani juu ya ekolojia ya eneo analo hudumia na mazao yanayozalishwa katika eneo lake, Pia tunawapatia shamba la Hekari moja ambalo analitumia kutoa elimu kwa wakulima katika eneo lake.

Suala la taarifa juu ya afya ya udongo limekua halifiki kwa mkulima na hata suala hili likienda kwa mkulima linaenda kwa lugha ngumu ambayo mkulima wa kawada hawezi kuelewa. Leo Mhe. Rais utagawa vipima afya ya udongo kwa halmshauri 143 nchi nzima.

# YALIYOZUNGUMZWA NA VIONGOZI WA KITAIFA WAKATI WA UZINDUZI WA UGAWAJI VITENDEA KAZI KWA MAAFISA UGANI KILIMO LEO APRILI 4, 2022 JIJINI DODOMA

## Mhe. Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa DODOMA



Sisi wana Dodoma tunakushukuru sana kwa jinsi ulivyowekeza pesa nyingi sana kwenye mkoa wetu katika mageuzi ya kilimo, kama timu tunakuhakikishia kuwa hatutakuangusha, tunaishukuru pia wizara kwa ushirikiano wao, tunaahidi kuwa mikakati yote tuliyojiwekea na kukubaliana Halmashauri za Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya kilimo msimu wa mwaka 2022/2023 tutaitekeleza ipasavyo.

## Mwenyekiti wa Tanzania Bankers Associations na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela



Tunawapongeza sana Wizara ya kilimo hasa kwa zana ya 'kilimo ni biashara' sekta ya fedha inafahamu umuhimu wa sekta hii kwani ndio sekta kubwa inayotoa ajira nchini, inachangia zaidi ya asilimia 26 ya pato la Taifa, na inafanya tuwe na chakula nchini cha kujitosheleza.

Sekta ya fedha kupitia Tanzania Bankers Associations tunatambua changamoto zilizopo kwenye kilimo hivyo tunaahidi kwamba tutahakikisha tunamshika mkono mkulima mmoja mmoja kwa kuongeza mnyororo wa thamani katika kilimo.

Naipongeza Serikali kupitia Benki ya kilimo Tanzania Agricultural Development Bank (TADB) kwa kuwa mdau mkubwa kuwezesha mabenki kutoa mikopo kwa wakulima kutoka Benki benki mbili tu Hadi sasa benki zinazotoa mikopo kwa wakulima zimefikia 14.

**Kwa hisani ya Idara ya Habari - MAELEZO**




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TFRA Prof. Anthony Mshandete (wa kwanza kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Mamlaka wakati wa unzinduzi wa ugawaji wa vitendea kazi kwa maafisa ugani kilimo nchini. Zaidi ya maafisa ugani 6100 watanufaia na vitendea kazi hivyo wapili kushoto ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo

# YALIYOZUNGUMZWA NA VIONGOZI WA KITAIFA WAKATI WA UZINDUZI WA UGAWAJI VITENDEA KAZI KWA MAAFISA UGANI KILIMO LEO APRILI 4, 2022 JIJINI DODOMA




Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo akiwa katika picha ya pamoja na viongozi walioshiriki siku ya unzinduzi wa ugawaji wa vitendea kazi kwa maafisa ugani kilimo nchini ambapo ya maafisa ugani 6100 watanufaia na vitendea kazi hivyo



Kaimu Meneja wa Kitengo cha Uhusiano, Mawasilisno na Elimu kwa Umma, Matilda Kasanga (Kushoto) na Kaimu Meneja wa Kanda ya Kaskazini Gothard Liampawe (Kushoto) wakiwa kwenye Maandalizi ya banda kwa ajili ya shughuli ya ugawaji wa vitendea kazi kwa maafisa ugani nchini uliofanyika tarehe 04.4.2022 jijini Dodoma na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Hassan Suluhu. Zaidi ya maafisa ugani 6000 watanufaika na vitendea kazi hivyo





Baadhi ya wananchi waliotembelea banda la TFRA leo tatehe 04.04.2022




Baadhi ya pikipiki zilizogawiwa kwa maafisa ugani nchini zikiwa katika uwanja tayari kwa ajili ya kuzinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan hafla iliyofanyika tarehe 4 Aprili, 2022.

# WASEMAVYO WADAU WA MBOLEA

Zamani utajiri ulikuwa unapimwa kwa wingi wa bidhaa zilizojaa kwenye maghala lakini wakati unabadilika, wakati tulionao sasa utajiri na heshma ya mtu unapimwa kwa kuona ana bidhaa gani katika ghala la kichwa chake. Mwalimu Nyerere aliwahisema uchi wanguoni mbaya lakini uchi wa akili ni mbaya zaidi uchi wa akili ni ile akili iliyokosa maarifa, unaweza ukafanya kazi za kilimo kwa kukatumia nguvu nyingi na muda mrefu bila maarifa utajikuta unavuna kidogo kuliko aliyetumia nguvu ndogo. Hapa tumepata fursa leo ya kupata maarifa mbalimbali juu ya kuimarisha kilimo chetu fursa hii tuitumie vizuri, ni fursa muhimu adimu na adhimu hakuna mtu aliyewahi kupata madhara kwa kutokana na maarifa kumzidia. Kwa hiyo hata kama wewe sio mkulima ni fursa nzuri ya kujifunza na kufahamu maana ukiwa na maarifa ni dhana bora katika maisha yako.

**Mwangi Rajab Kundya (Mkuu wa Wilaya ya Newala)**




**Niwapongeze sana kupata nafasi hii ya kujifunza juu ya matumizi sahihi ya mbolea. Elimu mliyoipata nasi tutakwenda kufanyia kazi nanyi pia mnapaswa kutumia elimu hii ili kuongeza tija katika shughuli zenu za kilimo.**

**Claudia Kitta Mkuu wa Wilaya ya Masasi**



# WASEMAVYO WADAU WA MBOLEA

Mimi nimekuja tofauti kabisa na wenzangu, Wenzangu wanaongea kilimo mimi naongea kuhusu anwani za makazi na sensa ya watu na makazi. Ndugu zangu mnajua Serikali ipo katika hatua za kuboresha anwani za makazi, tunaweka namba kwenye nyumba zetu, tunaipa mitaa majina na tunafanya shughuli zote za kufanya makazi yetu yawe yanapitika na kutambulika kirahisi. Niwaombe wananchi tushirikiane na Serikali ili zoezi hili lifanyike kwa ufanisi. Anuani za makazi zinakuja kurahisisha shughuli za sensa na makazi ifikapo mwezi Oktoba 23 wakati wa sensa. Anuani za makazi zinatusaidia katika kufikika, pia zitatusaidia wakati wa majanga. Kupitia sense na makazi tutajua Lilido kuna wazee wangapi na wa umri gani? Tutajua Lilido kuna walemavu wangapi na wanahitaji msaada, tutajua wananchi wa Lilido wanahitaji kituo cha afya au zahanati pia sensa ya watu na makazi itairahisishia serikali kazi wakati wa kupanga na kutekeleza mipango yake ya maendeleo. Ndugu zangu tulichelewa lakini tunataka tufike kwenye maendeleo kwa kuboresha makazi yetu, niwaombe sana wakati ukifika tutoe taarifa sahihi na tujiandae kuhesabiwa ifikapo Agosti 23, 2022. Mariam Khatib Chaurembo -

**Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu**




Katika kikundi chetu cha Tupendane tumejifunza mambo mengi kuhusu mtumizi sahihi ya mbolea tofauti na tulivyokuwa tunaelewa tunaahidi kuendelea kutekeleza kwa vitendo elimu hii tuliyoipata kwenye mashamba yetu pamoja na kuelimisha wakulima wenzetu. Katika scheme ya kilimo cha mpunga ya Kitere tunachangamoto mosi ni kuchakaa kwa kisima cha maji na mwingiliano wa matumizi kwa ajili ya kilimo na matumizi ya majumbani na hivyo kupelekea kujaza kisima hicho kwa kutumia muda mrefu sana Serikali itusadie kwa kutuchimbia visima kwenye maeneo yaliyowekwa alama kwa ajili ya kuchimba visima. Bei ya mbolea ni changamoto sana kwa mfano msimu uliopita mbolea tulinunua kwa shilingi 54 na baada ya muda ilipanda na kufikia 77 EGTna kwa sasa imefika hadi 118,000 na kutufanya kushindwa kumudu gharama hiyo hivyo tunaomba serikali kutupa ruzuku ili tuweze kutumia mbolea kwenye kilimo chetu na Zaidi tunaiomba TFRA kusimamia kikamilifu suala la upandishwaji holela wa mbolea nchini ili kuwakwamua wakulima.

**(Mtali Katibu kikundi cha tupendane)**



# KANDA YA KASKAZINI

## TFRA kanda ya kaskazini yaendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wasimamizi mipakani mwa nchi



Katika kuhakikisha elimu ya matumizi sahihi na biashara ya mbolea nchini inaeleweka kwa jamii, Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Kaskazini, Gothard Liampawe ameendelea kukutana na wadau katika maeneo tofautitofauti na kutoa elimu hiyo.

Awali, Liampawe akiambatana na Maafisa wengine kutoka katika ofisi yake tarehe 10 Aprili, 2022 alitembelea ofisi za Mpakani mwa Tanzania na Kenya za Holili na Tarekea kwa lengo la kujitambulisha pamoja na kujadiliana na watendaji mipakani humo juu ya masuala mbalimbali yanayohusu shughuli za udhibiti wa mbolea wanazoshirikiana hususani kwa mbolea zinazoingizwa nchini na kusafirishwa nje ya nchi.

Akizungumzia changamoto wanazokabiliana nazo kuhusu masuala ya mbolea, Mkuu wa Kituo cha PHS Holili Bw. Ajuaye Athuman amesema ni pamoja na uelewa mdogo juu ya mfumo wa Mbolea na Visaidizi vyake pamoja na taratibu za usajiri wa mbolea.

Pamoja na changamoto hizo, Bw. Athuman amesema changamoto nyingine ni ile inayotokana na mfumo kutokutoa nakala ngumu ya kibali cha Conditional release mara baaada ya kuipitisha/kuruhusu katika mfumo mteja anapokuwa amekidhi vigezo vya kuingiza mbolea yake kutoka nje ya nchi mara baada ya kukidhi vigezo kwa mujibu wa sheria ya mbolea No 9,2009 na kanuni zake za mwaka 2011.

Kwa upande wake Mkuu wa kituo cha PHS Tarakea Bw. Justine Michael Sikorey amesema kuna haja ya kupata mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo juu ya taratibu za usajiri wa mbolea kwani mafunzo hayo yatawasaidia kufanya maamuzi sahihi pindi wanapotekeleza majumu yao husussani kwa eneo la mbolea.

Pamoja ziara hiyo mapema tarehe 12 Aprili, 2022 Liampawe alifanya mafunzo kwa wadau wa mbolea 133 na kuwatunukiwa vyeti vitakavyowawezesha kufanikisha taratibu mbalimbali za usajili wa mbolea pamoja na kupata leseni ya biashara ya mbolea kwa mujibu wa sheria.

Mada mbalimbali zilifundishwa ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya mbolea, Elimu juu ya Super gro ilitolewa (kuwa si mbolea wala kirutubisho), Bei elekezi za Mbolea, Mfumo wa kieletronic wa Fis, Makatazo na maagizo mbalimbali yaliyotolewa na viongozi wa kisekta ikiwa ni pamoja na Waziri wa Kilimo Hussein Bashe na Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA Dkt. Stephan Ngailo yalioneshwa kwa njia ya Video.

Mafunzo hayo yalifanyika katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro katika ukumbi wa Kristu mfalme ulippo Moshi manispaa ambapo washiriki mbalimbali walihudhuria mafunzo hayo kutoka ya Mwanga,Same Simanjiro na Tanga.

# HABARI PICHANI





















Wajumbe wa bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kumaliza vikao vya bodi ambavyo hufanyika kwa mujibu wa sheria kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu ya mamlaka.





Wajumbe wa bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) wakiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Menejimenti ya mamlaka hiyo mara baada ya kumaliza vikao vya bodi vilivyofanyika kuanzia tarehe 26 hadi 28 Aprili, 2022 katika hoteli ya Morena Jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Bodi inayosimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Prof. Anthony Mshandete (kulia), Mkurugenzi wa (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo na wajumbe wa Bodi wakifuatilia mkutano baina yao na Waziri wa Kilimo Hussen Bashe (hayupo pichani) kilichofanyika katikaukumbi wa wizara Jijini Dodoma



Mjumbe wa Bodi ya TFC akieleza jambo wakati wa kikao baina ya Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe (hayupo pichani) na bodi za menejimenti za TFRA na TFC kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Wizara jijini Dodoma tarehe 29 Aprili, 2022.



Mjumbe wa Bodi inayosimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Charles Chenza akitoa maoni wakati wa kikao baina ya Waziri wa Kilimo, Husen Bashe (hayupo pichani) na bodi za menejimenti za TFRA na TFC kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Wizara jijini Dodoma tarehe 29 Aprili, 2022



Baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya TFRA wakifuatilia maelekezo ya Waziri wa Kilimo Hussen Bashe (hayupo pichani) wakati wa kikao baina ya TFRA, TFC na Waziri.